# <u>TANGAZO LA SERIKALI NA …….. LA TAREHE ………</u>

**SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA SURA 290**

**<u>SHERIA NDOGO</u>**

***Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)***

**SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA ZA MWAKA, 2025**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za Mwaka 2025, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali |
| Eneo la matumizi | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa |
| Tafsiri | 3. | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:<br><br>***"Afisa Mwidhiniwa"*** Maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br>"***Halmashauri"*** Maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>***"Kibali"*** Maana yake ni hati rasmi inayotolewa na Halmashauri kwa mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Shirika au Taasisi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi.<br>***"Madini ya Ujenzi"*** Maana yake ni mchanga, mawe, kokoto, tarazo, mawe meupe (quarts stone) chokaa, moram, tofali, marumaru nyekundu, soapstone, kifusi pamoja na madini mengine yanayotumika katika ujenzi.<br>***"Mkurugenzi"*** Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br>***"Ushuru"*** Maana yake ni malipo ya fedha yanayolipwa kwa Halmashauri kama tozo kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi ndani ya Mamlaka ya Halmashauri. |
| Ada na ushuru | 4. | 1) Halmashauri itaanzisha na kutoza ushuru wa madini ya ujenzi kutoka kwa kila mnunuzi wa madini hayo katika eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.<br>2) Ushuru huo utalipwa kwa Halmashauri au Wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo kuthibitisha malipo hayo. |
| Tathmini ya athari ya mazingira | 5. | 1) Itakuwa ni wajibu wa kila mchimbaji wa madini ya ujenzi na mwenye kibali au leseni kufanya tathmini ya athari ya mazingira na kuandaa mpango wa utunzaji wa mazingira kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Mazingira kabla ya kuchimba madini ya ujenzi**.** |

RASMI

| | | |
|---|---|---|
| Kibali | 6. | 1) Mtu yeyote, kikundi cha watu, Kampuni au Shirika wanaotaka kujishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi atatakiwa kuwa na kibali cha Halmashauri kinachomruhusu kufanya hivyo ndani ya eneo la Halmashauri.<br><br>2) Baada ya kufanya tathmini, endapo uchimbaji huo hauna athari kwa Mazingira na wakazi wa maeneo yanayochimbwa madini hayo, Halmashauri itatoa kibali cha kuruhusu uchimbaji wa madini hayo kitakacholipiwa ada kwa kiwango kilichoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.<br><br>3) Kibali kitakachotolewa na Halmashauri kitaeleza aina ya madini yanayochimbwa na eneo yatakapochimbwa madini hayo.<br><br>4) Halmashauri inaweza kufuta kibali kilichotolewa muda wowote endapo mchimbaji atakiuka masharti ya kibali hicho |
| Halmashuri kutenga maeneo ya uchimbaji | 7. | 1) Halmashauri itakuwa na jukumu la kutambua maeneo mbalimbali ya uchimbaji wa madini ya ujenzi ndani ya Halmashauri.<br><br>2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo ambayo hayajaruhusiwa na Halmashauri. |
| Halmashauri kumiliki leseni | 8. | 1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kisheria wa kumiliki leseni za uchimbaji wa madini ya ujenzi na kuuza madini yanayochimbwa katika maeneo husika.<br><br>2) Bila kuathiri kifungu cha 8(1) hapo juu, Halmashauri itaendelea kukusanya ushuru wa madini ya ujenzi yaliyochimbwa katika maeneo yenye leseni zinazomilikiwa na Halmashauri.<br><br>3) Kwa idhini ya Baraza la Madiwani, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuingia mikataba ya kisheria na mtu, kampuni, kikundi cha watu, taasisi au mwekezaji yeyote ambaye ataonyesha nia ya kuchimba madini ya ujenzi na kuuza katika maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri kwa leseni halali.<br><br>4) Halmashauri inaweza kuingia ubia na Serikali za vijiji katika maeneo yanayomilikiwa na vijiji kwa kuingia mikataba kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi katika maeneo ya vijiji na kugawana mapato yanayotokana na madini ya ujenzi katika maeneo hayo kulingana na mkataba wa ubia. |
| Kuwasilisha Taarifa za mapato | 9. | 1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika linalojishughulisha na uchimbaji wa madini ya ujenzi kutoa taarifa ya mapato yake ya mwaka au mwezi kama itakavyoelekezwa na Halmashauri. |

RASMU

| | | |
|---|---|---|
| | | 2) Afisa Mwidhiniwa ana wajibu wa kuhakiki mapato yatokanayo na shughuli husika kama mapato yana uhalisia na kile kinachopatikana |
| Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa | 10. | 1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote zinapofanyika shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi wakati wa saa za kazi kwa lengo la kufanya ukaguzi au kukusanya takwimu sahihi za uchimbaji wa madini unaofanyika katika eneo hilo. |
| Marufuku | 11. | 1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote, kikundi cha watu, Kampuni au Shirika kununua, kuuza, kutafiti, kuchimba au kusafirisha madini ya ujenzi bila kuwa na kibali halali cha Halmashauri kwa madhumuni hayo. |
| Kufifilisha kosa | 12. | 1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000/=) kwa mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatishwa katika Jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi. |
| Adhabu | 13. | 1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatakana na hatia atatozwa faini isiyopungua shillingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shillingi milioni moja (1,000,000) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo. |

## JEDWALI LA KWANZA

***(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 6(2)***

**ADA YA VIBALI**

| NA | AINA YA KIBALI | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuchimba na kuuza mawe mchanga | 200,000.00 |
| 2. | Kibali cha kuchimba udongo (kifusi) | 300,000.00 |
| 3. | Kibali cha kuchimba na kuponda kokoto | 400,000.00 |
| 4. | Kibali cha kuchimba madini ya chokaa | 350,000.00 |
| 5. | Kibali cha kuchimba na kuponda changarawe | 500,000.00 |
| 6. | Kibali cha kuchimba madini mengine ya ujenzi | 150,000.00 |

RASIMU

**<u>JEDWALI LA PILI</u>**

***(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4(1)***

**ADA NA USHURU WA MADINI YA UJEZI**

| NA | AINA YA MADINI | $M^3$ 1-5 | $M^3$ 5.1-10 | $M^3$ 10.1-15 | $M^3$ 15.1-20 | $M^3$ 20.1 - 25 | $M^3$ 25.1 - 30 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mchanga, changarawe, udongo wa kifusi, mawe, kokoto, chipings, crusherun na tofali za kuchoma | 5,000/= | 10,000/= | 15,000/= | 20,000/= | 25,000/= | 30,000/ |
| 2 | Mawe ya urembo yasiyochongwa (soapstone, quarts, redmable mika na mengineyo | 15,000/= | 25,000/= | 30,000/= | 35,000/= | 40,000/= | 50,000/= |
| 3 | Chokaa kg 25 | | | | | @500/= | |
| 4 | Ada ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi (kwa wasio na leseni) | | | | | Sh.200 @ mita ya mraba | |

RASIMU

RASIMU

## HATI YA KUKIRI KUTENDA KOSA

**(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 12 (1)***

Mimi:…………………………nakiri mbele ya Bw/Bi:……………………..Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kwamba Mnamo tarehe:…ya Mwezi:…mwaka:…….niliteda kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka, 2025.

Nipo tayari kulipa kiasi cha faini kinachodaiwa ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 12 (1) cha Sheria Ndogo hizo.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Jina:………… …Saini:… …. Alama ya dole gumba……………………………………Tarehe:………………
Mbele ya Ushahidi wa:
Jina…Saini:…………………… Alama ya dole gumba…………………………………Tarehe:………………………

Maelezo Mafupi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Jina la Mkurugenzi……………...............Saini.............................Tarehe………………
Muhuri………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe………………………………….. mbele ya:-

…………………………………………..
ROBERT MASUNYA
Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Iringa

…………………………………………….
STEPHEN MHAPA
Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Iringa

**NAKUBALI**
………………………………………
MOHAMED MCHENGERWA
**WAZIRI WA NCHI OR -TAMISEMI**